**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Mkuu wa Shule :0757808130**
**Makamu Mkuu wa shule:0719218249/0768636865**

**SHULE YA SEKONDARI MAGINGO,**

**S.L.P 20,**

**MADABA-RUVUMA.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
…………………………………………...................……………………………………………….....

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAGINGO HALMASHAURI YA MADABA MKOA WA RUVUMA**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha tano katika Shule hii mwaka 2026 na atasoma tahasusi ya.................................................

Shule ya Sekondari **MAGINGO** ipo umbali wa Kilometa 114 kutoka Songea Mjini. Pia shule ipo umbali wa KM 7 kutoka makao makuu ya Halmashuri ya wilaya ya Madaba. Aidha Usafiri wa basi toka Songea Mjini au toka Dar Es Salaam utashukia Kijiji cha Magingo kituo cha Tandale. kutoka kituo cha Tandale kuna umbali wa kilomita 1 hadi kufika shuleni ambapo unaweza kutembea au kutumia usafiri wa pikipiki au bajaji.

Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe .............Mwisho wa kuripoti ni tarehe ......... toka kutangazwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMIi tarehe ya kuripoti.

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

2.1 **Sare za Shule**

**Mambo muhimu ya kuzingatia:-Sare ya shule**

i. Mwanafunzi aje na sketi mbili za kijani-(rangi ya kijani namba 1039) (Sample ya kitambaa imeambatanishwa). Sketi ziwe ndefu kutoka kwenye kisigino mpaka kwenye pindo la sketi lisizidi sentimeta18 au inchi 7 ½. Aidha, **kwa atakayependa sketi zinapatikana karibu na shule kwa gharama ya sh.35,000/= kwa sketi 2**

ii. Sketi zake zisiwe na (belt) mkanda mpana, upana wa belt usizidi sentimeta 05 au inchi moja na nusu.

iii. Tai fupi rangi ya sketi (kijani) yenye alama ya V nyeupe.

iv. Marinda – pembeni pande zote mbele na nyuma marinda madogo matatu, katikati rinda box moja au rinda pana moja. Sketi isibane iwe na upana wa kutosha. Mchoro wa mshono wa sketi umeambatanishwa na barua hii.

v. Sketi ziwe ndefu sana, na siyo fupi zingatia urefu wa sentimeta 18 au inchi 7 ½ kutoka kwenye kisigino mpaka kwenye pindo la sketi.

vi. Mzazi/mlezi na mwanafunzi tafadhali zingatia vipimo hivyo, mwanafunzi atakaye shona na kuja na sketi/shamba dress kinyume na vipimo, rangi na aina ya kitambaa tulichoelekeza hatapokelewa, atarudishwa nyumbani ili aje na sare zilizoelekezwa kwa gharama zake.

vii. Mchoro wa mshono wa gauni umeambatanishwa.

viii. Mwanafunzi aweke alama ya jina lake na la mzazi wake kwenye sare na vitu vyake vyote kuepuka kuibiwa/kupotea. (**ALAMA IWEKWE NDANI YA BELTI**)

ix. Shati 2 nyeupe (Tomato) mikono mirefu.

x. Tai 2 fupi za Kufunga rangi ya kijani (kijani namba 1039) inayofanana na sketi.

xi. Viatu vya shule ni Juma na Roza visiwe na kisigino (angalia picha)

xii. Soksi nyeupe jozi 2 au zaidi

vi. Blazia nyeupe za kutosha

vii. Nguo za ndani za kutosha

viii. Sweta 2 -rangi ya damu ya Mzee (damu ya mzee) shingo ya V

ix. Nguo za kushindia (shamba dress) gauni 2 ndefu ikaribie kwenye kisigino mshono wa solo rangi ya dark blue na kijuba cha rangi ya dark blue (kwa wenye imani ya kiislamu)

x. Mwanafunzi aje na T-shirt ya shule rangi ya blue yenye nembo na moto wa shule. Tshirt hiyo hupatikana shuleni kwa sh. 15,000/=(Elfu kumi na tano tu).

xi. Kanda mbili/ndala kwa ajili ya kuogea rangi ya Blue/ nyekundu(Umoja)

xii. Kanga Doti moja (1) kwa ajili ya kuogea

xiii. Tranka 1 kubwa lenye kufuli imara

xiv. Begi dogo la mgongoni kwa ajili ya kubebea daftari

xv. Taulo la kujifutia baada ya kuoga

xvi. Miswaki, dawa za meno za kutosha

xvii. Nguo za michezo: Track suit ya dark blue yenye michirizi myeupe isiyo ya kubana, raba Nyeusi, Jezi ya timu ya Taifa rangi ya Blue.

xviii. Passport size 1 ya mwanafunzi mwenyewe kwa ajili ya kuweka kwenye faili lake. Passport 1 ya baba/mama/mlezi na 3 za ndugu wa karibu.

2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari 15 Quire 3 au 4, Peni za kutosha, penseli, rula ndefu, mkebe, kamusi

ii. Ream (A4) ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka. iii. Cheti halisi na nakala ya cheti cha kuzaliwa, cheti halisi na nakala ya cheti cha Kuhitimu kidato cha nne (Leaving certificate), cheti halisi na nakala ya matokeo ya kidato cha nne (Result slip)

iv. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (Oroodha imeambatishwa);

v. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

vi. Scientific Calculator kwa wanafunzi wanaosoma Basic mathematics na Geography

vii. Godoro futi 2 ½

viii. Mashuka Jozi 2 rangi ya pink, blanket 1, foronya ya godoro 1 rangi ya pink, chandarua 1 rangi nyeupe ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

xi. Kwanja 1, jembe 1 lenye mpini, reki 1, chelewa 1, fagio laini 1 (soft broom), fagio ngumu 1 (Hard broom), rubber squeezer 1, na brush ya chooni 1.

xii. Sabuni ya chooni lita 1

xiii. Koti la maabara 1(lab.coat) rangi nyeupe kwa wanaosoma masomo ya sayansi

xiv. Mwamvuli na koti la mvua jeusi (rain coat)- kwa mzazi anayejiweza xv. **Kitambulisho Cha NIDA** au **namba ya NIDA** ni muhimu sana kwa wenye umri wa zaidi ya miaka 18.

2.3 **Michango mbalimbali**

| **NA** | **AINA YA MCHANGO** | **KIASI** |
|---|---|---|
| **1** | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000 |
| **2** | Tahadhari | 5,000 |
| **3** | Nembo | 5,000 |
| **4** | Kitambulisho cha Shule | 5,000 |
| | **JUMLA** | **80,0000** |

**Michango yote ilipwe benki kwenye Akaunti ya shule NMB 6181200091 au 61801200091 MAGINGO SECONDARY SCHOOL RECURRENT.**

Kabidhi Risiti ya benki kwa mhasibu ili upewe Risiti ya shule pindi utakapofika shuleni

NB: Gharama za matibabu ya mwanafunzi ni jukumu la mzazi au mlezi mweneyewe.

Kwa asiye na kadi ya Bima ya afya aje na tsh. 50,400/= tu taslimu siku anapowasili ili apewa kadi ya Bima ya afya kwa mwaka mmoja.

3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamri kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (Preparation); iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule; vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa; viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; ix. Kutunza mali za shule
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- Ni marufuku kwa mwanafunzi kuleta vifaa vifuatavyo shuleni SIMU au KIFAA CHOCHOTE CHA SIMU, Pasi ya umeme, Camera, “Heater”, Smart Watch, pamoja na VYAKULA vya aina yoyote na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza vifaa tajwa hapo juu.
- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

- Usitume fedha kwa mtu USIYEMFAHAMU - atakayekupigia au kukuandikia ujumbe kuwa yeye ni mwalimu na kwamba yupo na mwanao/mwanafunzi hospitali anaumwa sana au ameanguka ghafla na kuvunjika. KWA MSAADA ZAIDI WASILIANA NA MKUU WA SHULE AU MATRON
- Ukitumiwa ujumbe unaohitaji utume pesa kwenye namba ya simu usiyoijua upuuze ujumbe huo.
- Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani nje ya zile ulizoagizwa na shule au kuvaa kofia, mizura, kufuga kucha ndefu, kupaka rangi kucha na midomo, kuvaa heleni, mikufu, bangili, nguo za kubana, viatu vyenye visigino virefu, mapambo mengine yoyote akiwa shuleni.

3.2 **Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamri kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule
vi. Kusuka nywele kwa mtindo wowote. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni .
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule. xiv. Kudharau Bendera ya Taifa xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

MKUU WA SHULE MAGINGO SEKONDARI S.L.P 20 MADABA

................................

**MWL KUNEMKA, S. M**

**MKUU WA SHULE**

4. **VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU** 1. **FOMU YA KUKUBALI AU KUKATAA KUJIUNGA NA SHULE HRI**

**1.1 MWANAFUNZI**

i. Majina kamili (matatu) ………………………………………………………………………………………

ii. Shule ya O-Level aliyosoma ……………………………………………………………………………………

iii. Namba ya mtihani (CSEE) ……………………………………………………………………………………

iv. Tarehe ya kuzaliwa ……………………………………………………………………………………

v. Nakubali/sikubali nafasi niliyopewa (kata lisilohusika)

vi. Nakiri/naahidi kutomiliki au kutumia simu shuleni, kutoshiriki mgomo, fujo na makosa ya jinai.

Sahihi ya mwanafunzi ………………………………Tarehe..............................

1.2 **MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

Jina la mzazi/Mlezi......................................Namba ya simu............................... Kazi ..................kijiji/mtaaa ........................... kata/shehia..................... Wilaya..................... mkoa............................

a) Nakubali mwanangu apate elimu yake hapo shuleni

b) Na kwamba afuate sheria na maelekezo yote, vinginevyo aadhibiwe

c) Na kwamba mwanangu alelewe katika dini ya ......................................................

d) Na kwamba siafiki yeye kumiliki au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule

e) Na kwamba nitampa mahitaji yote yaliyoainishwa

f) Na kwamba sitomhamisha mwanangu bila sababu ya msingi

**Sahihi ya Nzazi/ mlezi..............................Tarehe......................................**

1.3 **AFISA MTENDAJI WA KATA/KIJIJI/MTAA**

Jina …………………….......  Kijiji/kata/mtaa …………………….. Wilaya …………..….Mkoa……………………

Nathibitisha kuwa mwanafunzi ni wa kijiji/mtaa huu na ni raia wa Tanzania.

**Saini na Muhuri .................................................. tarehe.........................................**

## 2. TAARIFA KAMILI ZA MWANAFUNZI

1. Jina kamili ………………………………………………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa………………Dini........................Dhehebu……………………………
3. Mahali ulipozaliwa ……………………………………………………………………...
4. Shule ya msingi uliyosoma................................mwaka uliomaliza………………….
5. Shule ya sekondari uliyosoma...................................mwaka uliomaliza………………
6. Kidato unachokuja kuingia hapa Magingo sekondari…………………………………..
7. Jina la Baba/mlezi………………….………….…… Uhusiano ………………..Kazi ya baba/mlezi …………………… Dini……….………Namba ya simu……………………….…… E-mail …………....................Anuani…………………Kijiji/Mtaa/kitongoji/…………Na. ya nyumba………… Kata …………………….. Tarafa ……………… wilaya ……………….. Mkoa …………………

8. Jina la mama/mlezi........................Uhusiano…………….Kazi ya baba/mlezi………Dini ……………………. Namba ya simu ……....………… Email..........................Anuani……………..… Kijiji/Mtaa/kitongoji/Na. yanyumba …………….. Kata ……….. Tarafa …………… wilaya ………………….. Mkoa ……………

9. Kazi yoyote ya uongozi uliyowahi kufanya:-

10. **NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI; KAMA- DADA, KAKA, MJOMBA, SHANGAZI NK.**

Majina ya watu watatu wanaoruhusiwa kumchukua mtoto wako baada ya kuitwa na uongozi wa shule. (kumbuka hakuna siku ya kuwatembelea wanafunzi)

| S/N | JINA | UHUSIANO | MAHALI NAPOISHI | ANUANI NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |

**NB: Ndugu/Mlezi/Mzazi wa mwanafunzi atakayetambulika shuleni ni yule tu ambaye taarifa zake zimejazwa katika fomu hii na si vinginevyo**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**MAGINGO SECONDARY SCHOOL,**
**S.L.P 20,**
**MADAB-RUVUMA**
**……………….**

**To THE MEDICAL OFFICER,**

.................................................................

Please examine.............................................................................................

As to her fitness for pursuing further education at this school,

1. Haemoglobin ............................................................................................
2. P.V. Bleeding ...........................................................................................
3. (a) Sight defect .........................................................................................
   (b) Hearing..................................................................................................
4. Blood Pressure..........................................................................................
5. Urine for Sugar and Pregnancy test..........................................................
6. Stool for routine examination.....................................................................
7. Asthma.......................................................................................................
8. Skin diseases..............................................................................................
9. Leprosy .....................................................................................................
10. Epilepsy....................................................................................................
11. Pulmonary tuberculosis............................................................................
12. Deformity..................................................................................................
13. Mental Problem........................................................................................
14. Comments.................................................................................................

**MEDICAL CERTIFICATE**

**(To be completed by the Medical Officer)**

I have examined the above named and consider that she/he is mentally and physically fit for studies.

Signature ........................................................... Date ...........................................................

Designation ......................................................... Station ......................................................

**NB: (Fomu hri irudishwe Kwa Mkuu WA Shule ikiwa imejazwa)**

**.....................**
**S.M. KUNEMKA**
**HEADMASTER**
**MAGINGO SECONDARY SCHOOL**

## OORDHA YA VITABU MUHIMU KWA KILA SOMO

Unashauriwa kumnunulia mwanao vitabu kulingana na masomo anayosoma. Orodha ya vitabu unavyoweza kumnunulia/vinavyotakiwa kwa kila idara ni kama ifuatavyo:

### ACADEMIC COMMUNICATION

- Academic Communication By Tanzania Institute of Educatio (TIE)

### HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI

- Historia Ya Tanzania Na Maadili By Tanzania Institute of Educatio (TIE)

### HISTORY

1. History For Secondary Schools Form five & Six. By Tanzania Institute of Education.
2. Essentials in Advanced Level History Paper I & 2. By Saleh Yassin.
3. Major issues in African History by Tanzania Institute of Education
4. History of Modern Europe by Peacock
5. How Europe underdeveloped Africa by W. Rodney
6. History in focus: Modern World History by Ben Walsh
7. Mastering Advanced level History book two, by Kato, A (2011).

### GEOGRAPHY

1. Physical Geography For Adavance Secondary Schools – form five & Six - By Tanzania Institute of Education.
2. Practical Geography For Adavance Secondary Schools – form five & Six - By Tanzania Institute of Education.
3. Human Geography For Adavance Secondary Schools – form five & Six - By Tanzania Institute of Education.
4. Principles of Physical Geography by Monkhouse (2008)
5. Research methodology, Methods and Techniques. By C. R. Cothari.
6. Landforms in Africa by Collin Buckle
7. Map Reading by Mac Master
8. Human and Economic Geography by C. Morgan (1982)
9. Geography, An integrated Approach; Fourth edition by David Waugh (2009)
10. Practical Geography for Africa by John M. Pritchard (1990)

11. Map Reading, General Publications Ltd.- DSM by Durra, S.E.(2003)
12. R.B. Bunnet (2007) General Geography in diagrams

**kiswahili**

**(a) RIWAYA**

- Vuta N'kuvute
- Mfadhili
- Usiku Utakapokwisha

**(b) TAMTHILIYA**

- Kivuli Kinaishi.
- Morani.

**(c) USHAIRI**

- Kimbunga
- ChunguTamu
- Fungate ya Uhuru

**(d) SARUFI**

- Samakisa
- Samikisa
- Kitangulizi cha Tafsiri by Mwansoko.

  Nadharia ya Lugha by Nyangwine. - Kamusi ya Kiswahili Sanifu.

**GENERALSTUDIES**

- **Understanding GeneralStudies for Advanced Level** byJoannesBigirwamunguand Sospeter M. Deogratias.
- **General Studies for Advanced Level Certificate Form Five and Six** byRichardR.F Mbalase.

**BIOLOGY**

1. Dissecting kit
2. Biology for Advanced Level Secondary schools – Student'S Book for Form Five and Six (Tanzania Institute of Education).
3. New understanding Biology for A-level student by Glenn & s. Toole (1999)
4. Systematic and classification by L.K. Msaki (1993)
5. Biology, A functional Approach by M.B.V Roberts (1971)
6. Advanced Biology: Principle and Application by C.J. Clegg & D.G. Mackean (2000)
7. Biological Science by Taylor, etal (1997
8. S. Chand's Biology for class XI & XRI by P.S Verma & B.P Pandey (2005).
9. Guide to dissection by H.G.Q Rowett (2005)

**CHEMISTRY**


1. Physical chemistry for Advanced Level Secondary schools – Student'S Book Form Five and Six (Tanzania Institute of Education)
2. Inorganic chemistry for Advanced Level Secondary schools – Student'S Book Form Five and Six (Tanzania Institute of Education)
3. Organic chemistry for Advanced Level Secondary schools – Student'S Book Form Five and Six (Tanzania Institute of Education)
4. General chemistry for Advanced Level Secondary schools – Student'S Book Form Five and Six (Tanzania Institute of Education)
5. Advanced Chemistry Physical and industrial by P. Mathew (2006)
6. Essentials of physical chemistry by Arun Bahil, B.S Bahil & G.D Tuli (2012).
7. Organic Part A & B by A. Abdullah & M.H. Nkunya.
8. Inorganic Part A & B by J.S Maro Guterman & M. Mikesewala (1989)
9. Physical Chemistry by Ddungu& J.B.A Mihigo (1998)
10. Advanced level Inorganic Chemistry PART I & RI by Tanzania Institute of Education (1995)
11. Organic Chemistry an introduction by Jack E. Fernandez (1982)
12. Understanding Chemistry for A-level student
13. Conceptual chemistry for class XRI& XI by S.K Jaini (2011).
14. Advanced level chemistry, fourth edition by E.N Ramsd

**KIATU JUMA NA ROZA**



**SKETI ZA DARASANI(ZIWE MBILI)**

**NB:Mchoro huu hapa chini unaonyesha namna ya mshono**




**MCHORO WA SHAMBA DRESS**

